

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA



Mkuu wa TAKUKURU (M) Kinondoni.
S.L.P 90397, Kinondoni
Simu : 222170852 Nukushi 2170963
Mob. 0738159236, 0652409165
Barua pepe: rbckinondoni@pccb.go.tz
Wavuti www.pccb.go.tz

TAARIFA KWA UMMA

UTENDAJI KAZI WA TAKUKURU MKOA WA KINONDONI KWA KIPINDI CHA APRIL, 2020 – JUNI, 2020.

Ofisi ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Mkoa wa Kinondoni kwa kipindi cha miezi mitatu April 2020 hadi Juni 2020 imeweza kutekeleza malengo yake ya utendaji kazi kama yalivyoainishwa kwenye Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na 11/2007.

Ofisi hii ipo eneo la Magomeni usalama/makuti, na ina jukumu la kuchunguza, kuelimisha na Kuzuia rushwa katika maeneo yote ya Manispaa ya Kinondoni pamoja na Manispaa ya Ubungo.

UCHUNGUZI

TAKUKURU Mkoa wa Kinondoni kuanzia mwezi April 2020 hadi Juni 2020 imeweza kutekeleza majukumu yake kwa kupokea Taarifa Mpya, kufungua kesi mpya kuendesha kesi zilizokuwa zimeshafunguliwa, kufungua majalada mapya ya Uchunguzi na kuendelea na Uchunguzi wa majalada ya zamani kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali hapo chini:

S/N	Taarifa za malalamiko, Majalada na Kesi	IDADI
1.	Malalamiko yaliyopokelewa	156
2.	Majalada yaliyopelekwa Makao Makuu (HQ)	14
3.	Majalada yaliyorudi na kibali cha DPP	3
4.	Kesi mpya zilizofunguliwa Mahakamani	3
5.	Kesi zinazoendelea Mahakamani	20
6.	Kesi zilizoshinda	2
7.	Kesi zilizoshindwa	1
8.	Fedha zilizoookolewa	56,792,200

Mafanikio haya ya utekelezaji wa jukumu la kuchunguza taarifa za vitendo vya rushwa yametokana na mwitikio mzuri wa Jamii katika kutoa taarifa na utayari wa kuipa TAKUKURU ushirikiano. Taarifa **156** zimepokelewa kutoka kwa wadau mbalimbali ambao ni vyombo vya habari, vyombo vya ulinzi na usalama, Idara na Taasisi mbalimbali pamoja na watu binafsi ambapo kati ya taarifa hizo majalada **9** yalifunguliwa, Idara zilizoongoza kwa kulalamikiwa ni **TAMISEMI, Idara Binafsi, Polisi na Mahakama.**

ELIMU KWA UMMA

Kwa upande wa Uelimishaji Umma, katika kipindi hicho cha kuanzia April 2020 hadi Juni 2020, TAKUKURU (M) Kinondoni iliweza kutoa Semina 5 kwa Watumishi wa Umma na wa Taasisi binafsi wa Mkoa wa Kinondoni, wapatao 510 walipata elimu ya Rushwa ikiwa ni pamoja na kufahamu maana ya Rushwa, sababu ya kuwepo kwa Rushwa, Madhara ya Rushwa/ madhara ya Rushwa ya ngono na jukumu na umuhimu wa jamii kushiriki katika mapambano dhidi ya Rushwa hasa wakati wa uchaguzi.

TAKUKURU (M) Kinondoni pia iliweza kuendesha Mjadala wa wazi 1 uliohusu rushwa ya ngono kwa wanafunzi wa vyuo vya elimu ya juu na uliohudhuriwa na wanafunzi wapatao 200 kutoka vyo vya NIT, UDSM, TUDARCO, ARDHI pamoja na Chuo cha ustawi wa jamii(ISW).

TAKUKURU Mkoa wa Kinondoni imeweza kuelimisha zaidi ya watu milioni 3 kupitia vipindi vya Televisheni vya UPENDO TV na Redio za UHURU FM, na UPENDO media kuhusu Mapambano dhidi ya rushwa hasa wakati wa uchaguzi,

UZUIAJI RUSHWA

TAKUKURU Mkoa wa Kinondoni pia imefanya udhibiti mbalimbali kwenye maeneo yaliyokua yakilalamikiwa sana na kuonekana kuwa na mianya ya rushwa iliyokua ikitumiwa na watumishi au uongozi wa eneo husika katika kupindisha sheria, taratibu na kanuni ili kujipatia manufaa binafsi.

Aidha kwa kipindi hicho, Mifumo sita (2) Mianya ya rushwa katika mfumo wa utatuzi wa migogoro ya ardhi kwenye Mabaraza ya ardhi ya kata Manispaa ya Kinondoni na Mianya ya Rushwa katika kushughulikia malalamiko ya ulawiti, unajisi na ubakaji kwa watoto katika Manispaa ya Kinondoni

Vilevile ili kuleta ufanisi zaidi katika utendaji kazi TAKUKURU (M) Kinondoni imefanya ufuatiliaji wa fedha/vifaa tiba na dawa za kampeni dhidi ya COVID 19 mkoa wa Kinondoni, ufuatiliaji wa mradi wa ukarabati wa madarasa 7 na ujenzi wa maabara 1 shule ya sekondari Kijitonyama, ufuatiliaji wa mradi wa ukarabati wa madarasa 4 shule ya sekondari Oysterbay, ufuatiliaji wa mradi wa ukarabati ukarabati wa madarasa 21 shule ya sekondari Magomeni. Miradi hiyo ilikuwa na thamani ya takribani TZS 332,000,000/=

HITIMISHO

Natoa wito kwa Wananchi wote kuendelea kushirikiana nasi katika mapambano dhidi ya Rushwa kwa kutoa Taarifa za vitendo vya rushwa kwa kufika ofisini au kwa kupiga simu namba 0652 409 165, 0738 159 236 au simu ya bure 113 au kutuma ujumbe mfupi kwenye namba 113. Aidha na waasa wananchi wote hasa wale ambao wana malengo ya kugombea nafasi mbalimbali wakati wote wa kipindi hiki. Kujihusisha na vitendo vya rushwa ni kosa jinai na TAKUKURU itawashughulikia wote watakao bainika kufanya vitendo hivyo.

**IMETOLEWA NA
E. HAZINAMWISHO
KAIMU MKUU WA TAKUKURU
MKOA WA KINONDONI
09/07/2020**

